JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**



# TAARIFA YA MCHANGO WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI KATIKA MAENDELEO YA TAIFA KWA MWAKA 2023

*Septemba, 2024*

# YALIYOMO

**YALIYOMO**

**VIFUPISHO**

**ORODHA YA MAJEDWALI**

**ORODHA YA MAUMBO**

**DIBAJI**

**SHUKRANI**

**MUHTASARI WA TAARIFA**

**SURA YA KWANZA**

**Msingi, Malengo na Walengwa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali........ 01**

Utangulizi ........ 01

Msingi wa Taarifa ........ 01

Malengo ya Taarifa ........ 02

Walengwa wa Taarifa ........ 02

Mawanda ya Uchambuzi ........ 02

Mbinu Zilizotumika ........ 02

**SURA YA PILI**

**Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Upande wa Tanzania Bara........ 03**

Utangulizi ........ 03

Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 03

Mfumo wa Kisheria wa Usajili na Uratibu wa Mashirika ........ 04

Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiseriakali ........ 04

Mkakati wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 05

Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika ........ 05

Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 06

Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 06

Vikao Kazi vya Kisekta kati ya Wizara na Mashirika ........ 06

Mahitaji ya Kisheria na Kikanuni Baada ya Usajili ........ 07

Uwasilishaji wa Taarifa na Ulipaji wa Ada ........................................................ 07

Uzoefu wa Nchi Nyingine katika Uratibu wa Mashirika .................................. 12

**SURA YA TATU**

**Mapato, Matumizi na Mikakati Mbalimbali ya Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali .................................................................. 13**

Utangulizi ........................................................................................ 13

Mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ...................................................... 13

Matumizi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali .................................................... 15

Mikakati ya Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ............................... 16

**SURA YA NNE**

**Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Katika Nyanja Mbalimbali za Maendeleo ......................................................................... 18**

Utangulizi ........................................................................................ 18

Utekelezaji wa Miradi na Afua Kisekta .......................................................... 18

Sekta ya Afya ........................................................................................ 20

Uwezeshaji wa Jamii Kiuchumi ................................................................... 20

Ulinzi wa Jamii ........................................................................................ 21

Uhifadhi wa Mazingira ............................................................................. 23

Sekta ya Elimu ........................................................................................ 25

Sekta ya Kilimo ........................................................................................ 26

Utawala Bora ........................................................................................ 26

Sekta ya Maji ........................................................................................ 27

Masuala ya Kijinsia ................................................................................. 28

Haki za Binadamu ................................................................................... 28

Wanufaika wa Miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali .................................. 30

Ajira Zilizozalishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali .................................... 32

Makato ya Kisheria ya Posho na Mishahara ya Waajiriwa .............................. 32

Utekelezaji wa Sera za Ndani ya Uendeshaji wa Mashirika ............................ 32

## SURA YA TANO

**Changamoto na Mapendekezo ya Kuboresha Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ........ 33**

Utangulizi ........ 33

Changamoto ........ 33

Mapendekezo ........ 34

Hitimisho ....... ........ 35

**REJEA ........ 36**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ACN** | Aid to the Church in Need |
| **ARAF** | African Rafiki Foundation |
| **AWF** | African Wildlife Foundation |
| **BOT** | Bank of Tanzania |
| **CCBRT** | Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania |
| **CDC** | Centre for Disease Control |
| **CEELS** | Community Economic Empowerment and Legal Support |
| **CIC** | Children in Cross fire |
| **DRC** | Danish Refugee Council |
| **EU** | European Union |
| **FCDO** | Foreign, Commonwealth and Development Office |
| **FCS** | Foundation for Civil Society |
| **GAC** | Global Affairs Canada |
| **GePG** | Government Electronic Payment Gateway |
| **GFFO** | German Federal Foreign Office |
| **IDYDC** | Iringa Development of Youth Disabled and Children Care |
| **IOP** | Ilula Orphan Program |
| **JMT** | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **KOICA** | Korean International Cooperation Agency |
| **MKIUMA** | Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali |
| **NaCoNGO** | National Council of Non-governmental Organizations |
| **NGOs** | Non-Governmental Organizations |
| **NIDA** | National Identification Authority |
| **NIS** | NGOs Information System |
| **NORAD** | Norwegian Agency for Development Cooperation |
| **NSSF** | National Social Security Fund |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa |

| | |
|---|---|
| **OSPC** | Open Society Policy Centre |
| **PATH** | Program for appropriate Technology in Health |
| **PAYE** | Pay As You Earn |
| **PEPFAR** | President's Emergency Plan for Aids Relief |
| **SDL** | Skills Development Levy |
| **SIDA** | Swedish International Development Cooperation Agency |
| **TBI** | Tanzania Bora Initiative |
| **THPS** | Tanzania Health Promotion Support |
| **UNFPA** | United National Population Funds |
| **UNHCR** | United Nations High Commission for Refugees |
| **UNICEF** | United Nations Children's Fund |
| **USAID** | United Nations Agency for International Development |
| **WCF** | Workers Compensation Fund |
| **WWF** | World Wide Fund for Nature |

# ORODHA YA MAJEDWALI

**Jedwali 2.2:** Usajili wa Mashirika kwa Mwaka 2023........................................ 03

**Jedwali 2.11.1:** Mashirika Yaliyowasilisha Taarifa kwa Ngazi ya Usajili .......... 07

**Jedwali 2.11.2:** Mashirika Yaliyowasilisha Taaifa kwa Ngazi ya Mkoa............. 08

**Jedwali 2.11.3:** Mashirika Yaliyolipa Ada kwa Ngazi ya Usajili.........................09

**Jedwali 2.11.4:** Mashirika Yaliyolipa Ada kwa Ngazi ya Mkoa..........................09

**Jedwali 2.11.5:** Mikataba Iliyowasilishwa na Kuidhinishwa............................ 10

**Jedwali 3.2:** Vyanzo vya Mapato ya Mashirika............................................... 14

**Jedwali 3.3:** Matumizi ya Fedha za Mashirika................................................ 15

**Jedwali 4.2:** Mchanganuo wa Fedha Kisekta.................................................. 19

**Jedwali 4.3:** Idadi ya Waliofikiwa na Miradi.................................................... 29

**Jedwali 4.4:** Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa............................................... 30

# ORODHA YA MAUMBO

**Umbo 2.2:** Usajili wa Mashirika kwa Mwaka 2023........................................ 04

**Umbo 2.11.5:** Mikataba Iliyowasilishwa na Kuidhinishwa ............................. 11

**Umbo 3.2:** Vyanzo vya Mapato ya Mashirika................................................ 14

**Umbo 3.3:** Matumizi ya Fedha za Mashirika................................................ 16

**Umbo 4.3:** Asilimia ya Waliofikiwa na Miradi................................................ 30

**Umbo 4.4.1:** Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa............................................ 31

**Umbo 4.4.2:** Mgawanyo wa Ajira kwa Jinsia................................................ 31

# DIBAJI

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ina jukumu la kusajili na kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unatekelezwa kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya Mashirika ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

Kama mnavyofahamu, Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeendelea kukua kwa kasi kutoka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,110 mwaka 2005 hadi Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 8,669 kufikia mwezi Desemba 2023. Ni matarajio ya Wizara yenye dhamana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yataendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji kama ilivyoainishwa katika Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara.

Kama sehemu ya jitihada za Serikali katika kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeandaa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023, ambapo pamoja na mambo mengine, imeainisha mchango wa Mashirika hayo katika utekelezaji wa miradi na afua za afya, uwezeshaji wa jamii kiuchumi, ulinzi wa jamii, elimu, kilimo, utawala bora, maji, jinsia, haki za binadamu, nishati na miundombinu.

Miradi na afua zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sio tu zimewanufaisha wananchi wa Tanzania kijamii, bali pia zimechangia katika kuboresha utoaji wa huduma za kijamii, kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, pamoja na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.
Aidha, katika kuhakikisha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaendelea kutoa mchango wake katika maendeleo ya Taifa, Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi ya utendaji kazi, ikiwemo kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuongeza Ramani ya Kidigitali ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambayo ni nyenzo muhimu itakayosaidia kutambua mahali yalipo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pamoja na miradi na afua zinazotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia teknolojia rahisi ya kiganjani.

Masuala mengine ni Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa, Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi, pamoja na Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 – 2026/27), ambao ulizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), tarehe 04 Oktoba, 2022 ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa tarehe 30 Septemba, 2021 wakati wa Kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kwa kuzingatia umuhimu na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, napenda kutoa wito kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia misingi ya uwazi na uwajibikaji, kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji baina yake na wadau wengine wa maendeleo, pamoja na kuhakikisha kunakuwepo na uendelevu wa Mashirika hayo hapa nchini. Ni matumaini yangu kuwa taarifa hii itakuwa chachu kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine kuendelea kutekeleza shughuli zao kwa uwazi na uwajibikaji.



Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe

**KATIBU MKUU**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# SHUKRANI

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inapenda kutoa shukrani za pekee kwa watu na taasisi mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyingine zimeshiriki katika mchakato wa upatikanaji wa rasilimali fedha, uwezeshaji, uandaaji, uhariri, usanifu, uchapishaji na usambazaji wa Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023.

Shukrani za dhati ziende kwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb); Katibu Mkuu, Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe; Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii na Makundi Maalum, Wakili Amon Mpanju; na Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Jinsia na Wanawake, Bi. Felister Mdemu, kwa kuiwezesha Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini.

Vilevile, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali chini ya Mwenyekiti wake, Hajjat Mwantumu Mahiza, kwa usimamizi na uratibu uliotukuka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa upande wa Tanzania Bara. Aidha, shukrani zilifikie Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) chini ya Mwenyekiti wake Bw. Jasper Makala na Katibu Mkuu wake Bw. Adamson Nsimba, kwa ushirikiano thabiti ambao wamekuwa wakiutoa kwa Wizara katika kuratibu na kusimamia sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini.

Vilevile, shukrani ziende kwa Menejimenti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maaalum kwa michango yao ya hali na mali iliyowezesha uandaaji na uboreshaji wa fani na maudhui ya Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023. Nawashukuru pia kwa maoni mliyoyatoa na kuridhia kwenu kuchapishwa kwa Kitabu hiki ili kiweze kutumiwa sio tu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, bali pia na Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Wanufaika wa Miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii ya Watanzania kwa ujumla.

Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Timu ya Wataalam iliyopewa jukumu la kuratibu uandaaji wa Kitabu cha Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023, wakiongozwa na Bw. Charles Komba (Mwenyekiti), Bw. Abraham Mushashu (Makamu Mwenyekiti), Bw. Faki Shaweji (Katibu) na Bi. Josephine Mchalange (Mratibu). Wajumbe wengine ni Dkt. Methusela Masanja, Bw. Julius Katemba, Bi. Gladness Mushi, Bw. Issa Mtinangi, Bi. Zafarani Zungiza, Bw. Jacob Melubo, Bi. Wende Saga, Bw. Dennis Bashaka na Bw. Tema Hassan. Nawashukuru sana kwa kazi nzuri na ya kutukuka mliyoifanya!

Mwisho, lakini sio kwa umuhimu, napenda kutoa shukrani za kipekee kwa Kampuni ya Speedy Print Limited, Shirika la ActionAid Tanzania, Shirika la Mpingo Conservation and Development Initiative (MCDI), Shirika la Trees for the Future Inc, Shirika la Ilula Orphan Program (IOP), Shirika la The Creator Share Foundation, Shirika la Tanzania Bora Initiative (TBI), Shirika la Plan International, Shirika la Iringa Development of Youth Disabled and Children Care (IDYDC), Shirika la African Wildlife Foundation, Shirika la Community Economic Empowerment and Legal Support (CEELS), Shirika la See Ability First International – Tanzania,

Shirika la Health and Insurance Management Services Organization (HIMSO), Shirika la Tanzania Peace, Legal Aid and Justice Centre (PLAJC), Shirika la The Tunu Pinda Foundation, Shirika la African Rafiki Foundation (ARAF) na Shirika MIICO kwa kuwezesha uandaaji, uhariri, usanifu na uchapishaji wa nakala za Kitabu hiki.



Vickness G. Mayao

**MSAJILI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE
NA MAKUNDI MAALUM**

# MUHTASARI WA TAARIFA

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni miongoni mwa wadau muhimu wa kimkakati katika jitihada za kuwaletea wananchi maendeleo na kuimarisha ustawi wa jamii ndani na nje ya Tanzania. Kwa upande wa Tanzania Bara, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ina jukumu la kuratibu Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mujibu wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kufuatia hali hiyo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekuwa ikiandaa taarifa ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwa sehemu ya nyenzo muhimu ya kupima utendaji kazi wa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mwaka husika. Hivyo, Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2023 imegawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza imejikita kuelezea kuhusu msingi na malengo ya kuandaliwa kwa taarifa hii, walengwa wa taarifa, pamoja na mawanda na mbinu zilizotumika katika uandaaji wa taarifa hii.

Sura ya Pili imejikita kuelezea kuhusu usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kubainisha mfumo wa kisheria wa uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwa ni pamoja na Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara, Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na vikao kazi vya kisekta kati ya Wizara na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Sura ya Tatu ya taarifa hii imejikita kuelezea kuhusu mapato, matumizi na mikakati mbalimbali ya uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo kupitia uchambuzi wa taarifa za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,368, imebainika kuwa jumla ya Shilingi 2,614,880,491,980 kilipokelewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kwamba kiasi cha Shilingi 2,461,926,876,419 kilitumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za kiutawala

Sura ya Nne ya taarifa hii imejikita kuelezea mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali, ambapo sekta iliyoongoza kwa mwaka 2023 ilikuwa ni Sekta ya Afya, ikifuatiwa na Uwezeshaji wa Jamii Kiuchumi na Ulinzi wa Jamii. Sekta nyingine ni pamoja na Uhifadhi wa Mazingira, Sekta ya Elimu, Sekta ya Kilimo, Utawala Bora, Sekta ya Maji, Masuala ya Jinsia na Haki za Binadamu.

Sura hiyo imeelezea pia kwa kina kuhusu makundi yaliyonufaika zaidi na miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo wanawake walifikiwa kwa asilimia 47.4 na vijana walifikiwa kwa asilimia 30.5. Jumla ya taasisi 4,089,773 zikiwemo za Serikali na Sekta Binafsi zilifikiwa katika kipindi husika. Aidha, Mashirika 205 yalichangia kiasi cha Shilingi 42,603,379,942 kupitia makato ya PAYE, Mashirika 267 yalichangia kiasi cha Shilingi 30,873,522,541 kupitia makato ya NSSF, Mashirika 112 yalichangia kiasi cha Shilingi 2,816,947,325 kupitia makato ya SDL na Mashirika 240 yalichangia kiasi cha shilingi 1,154,751,310 kupitia makato ya WCF.

Sura ya Tano imejikita kuelezea kuhusu changamoto mbalimbali katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwemo changamoto ya baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutowasilisha taarifa na wengine kushindwa kutumia Mfumo wa NIS.

Changamoto nyingine ni upatikanaji wa rasilimali fedha na uwepo wa baadhi ya kodi zinazotozwa kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA).

Baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa katika sura hiyo ni pamoja na kuendelea kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuhusu matumizi ya Mfumo wa NIS na uwasilishaji wa taarifa, kujenga, kuimarisha na kuboresha mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, pamoja na kutumia fursa ya huduma zinazotolewa na Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi (Tax Ombudsman Service Tanzania - TOST), ambayo ina jukumu la kupitia na kushughulikia malalamiko yote ya walipakodi.

# SURA YA KWANZA

## Msingi, Malengo na Walengwa Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

### 1.1 Utangulizi

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ina jukumu la kusajili na kuratibu Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania. Aidha, Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 imeweka misingi ya uwazi na uwajibikaji kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na kuhimiza ubia kati ya Serikali na Mashirika hayo ili kutambua mchango wao kwa jamii.

Katika kutekeleza hilo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hutakiwa kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa kazi wanazofanya katika kipindi cha robo mwaka na mwaka ili kuwezesha utambuzi wa shughuli zilizotekelezwa pamoja na mchango wake katika maendeleo ya Taifa. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Wizara ya Fedha, Wizara, Idara na Taasisi za Kisketa, pamoja na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikifanya ufuatiliaji na tathmini ya shughuli au miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Kupitia ufuatiliji huo, Serikali na wadau mbalimbali hupata fursa ya kutathmini mchango unaotolewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa, pamoja na tija ya miradi inayotekelezwa na Mashirika hayo kwa jamii kwa kuzingatia sera, malengo na vipaumbele mbalimbali vya Taifa. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hujikita kupima mwenendo wa utekelezaji wa majukumu ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia sekta hiyo, ikiwemo kubainisha mafanikio na changamoto za kiutendaji katika Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini.

### 1.2 Msingi wa Taarifa

Katika kipindi cha miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na uhitaji wa taarifa sahihi za mchango wa sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka miongoni mwa wadau mbalimbali, ikiwemo Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Utafiti, Vyombo vya Habari, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii kwa ujumla.

Kufuatia hali hiyo, Kitabu cha Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa kilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 30 Septemba, 2021 wakati wa kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kilichofanyika Jijini Dodoma, ambapo alielekeza kazi ya uandaaji wa taarifa hiyo kuwa endelevu ili kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali.

## 1.3 Malengo ya Taarifa

Lengo kuu la uandaaji wa taarifa hii ni kutathmini ukuaji wa sekta na kupata picha halisi ya mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa kupitia taarifa za utekelezaji wa miradi na afua zilizowasilishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023. Malengo Mahsusi ni pamoja na:

**(a)** Kutambua kiwango cha rasilimali fedha kilichopokelewa na kutumiwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali.

**(b)** Kutambua idadi na aina ya miradi na afua zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023.

**(c)** Kutambua idadi na aina ya wanufaika wa miradi na afua mbalimbali zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023.

**(d)** Kutathmini utelekezaji wa sera na mikakati mbalimbali, ikiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 na Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2022/23 – 2026/27).

**(e)** Kubainisha fursa na changamoto katika uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa na wadau mbalimbali.

## 1.4 Walengwa wa Taarifa

Walengwa wa taarifa hii ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ambayo ni Wizara yenye dhamana ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pamoja na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Utafiti, Vyombo vya Habari, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii kwa ujumla.

## 1.5 Mawanda ya Uchambuzi

Uchambuzi huu umehusisha taarifa za utekelezaji na taarifa za fedha zilizokaguliwa ambazo ziliwasilishwa kwa ukamilifu na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,368 kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS), pamoja na taarifa ya zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya miradi na afua zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Njombe, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Singida, Tabora na Tanga.

## 1.6 Mbinu Zilizotumika

Mbinu zilizotumika katika uandaaji wa taarifa hii ni pamoja na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji na taarifa za fedha zilizokaguliwa, taarifa za robo mwaka na taarifa za mikataba ya ufadhili zilizowasilishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Njombe, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Singida, Tabora na Tanga.

# SURA YA PILI

## Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa Upande wa Tanzania Bara

### 2.1 Utangulizi

Kwa upande wa Tanzania Bara, usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unafanyika kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ambayo imetoa haki kwa wananchi kujumuika katika makundi mbalimbali, pamoja na Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001, ambayo imejenga msingi wa uwepo wa mfumo wa kisheria na kikanuni yenye lengo la kuongeza ufanisi katika uratibu wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.


### 2.2 Usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba 2023, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusajili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ambapo katika kipindi hicho, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,482 yamesajiliwa katika ngazi ya Kitaifa (1,355), Kimataifa (64), Mkoa (37) na Wilaya (26) na hivyo kufikisha jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 9,671 kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali 2.2 na Umbo 2.2 hapo chini:

*Jedwali 2.2: Usajili wa Mashirika kwa Mwaka 2023*

| Na | Ngazi ya Usajili | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 01 | Ngazi ya Wilaya | 26 | 1.80% |
| 02 | Ngazi ya Mkoa | 37 | 2.50% |
| 03 | Ngazi ya Kitaifa | 1,355 | 91.40% |
| 04 | Ngazi ya Kimataifa | 64 | 4.30% |
| | **Jumla** | **1,482** | **100.00%** |

*Umbo 2.2: Usajili wa Mashirika kwa Mwaka 2023*




## 2.3 Mfumo wa Kisheria wa Usajili na Uratibu wa Mashirika

Kwa upande wa Tanzania Bara, uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unatekelezwa kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2001 na Sheria ya Mashirika ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

Aidha, Kifungu cha 31(a) na (b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 kinayataka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza shughuli zao kwa kuzingatia sheria nyingine za Nchi, ikiwemo sheria za kodi, sheria za kazi na ajira, sheria za uhamiaji, sheria za kuzuia usafirishaji haramu wa binadamu, sheria za kupambana na ugaidi na utakasishaji wa fedha haramu, pamoja na uzingatiaji wa mila, desturi na utamaduni wa jamii inayowahudumia, ilimradi mila na tamaduni hizo hazikinzani na Sheria nyingine za Nchi.

## 2.4 Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Katika kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara yenye dhamana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) iliandaa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara (2020) ili kuondoa mgongano wa majukumu na kuimarisha uratibu wa pamoja wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Mwongozo huo ulizinduliwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mhe. Ummy Mwalimu (Mb), tarehe 17 Juni, 2020.

Kupitia Mwongozo huo, Wizara, Idara na Taasisi za Kisekta zina wajibu wa kuwezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutambua fursa na vipaumbele vilivyopo, kusimamia vigezo vya kitaalam na kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanatekeleza afua zinazoendana na malengo au vipaumbele vya Taifa. Kwa upande wake, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuwasiliana na Wizara, Idara na Taasisi za Kisekta ili kubaini maeneo yenye uhitaji na kupata mwongozo wa kisera kabla ya kuanza kwa utekelezaji wa miradi au afua.

## 2.5 Mkakati wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2022/23-2026/27 (National Strategy for NGOs Sustainability 2022/23-2026/27) ulizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), tarehe 04 Oktoba, 2022 wakati wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, ikiwa ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 30 Septemba, 2021 wakati wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Mkakati huo umelenga kujenga uwezo thabiti wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa na uhimilivu na kujitegemea kiuchumi, kuimarisha mazingira wezeshi ya ndani yatakayosaidia uendelevu wa muda mrefu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayofanya kazi nchini Tanzania, kupanuka kwa wigo wa mitindo ya ufadhili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kukidhi mahitaji yake ya ufadhili, pamoja na kuimarisha uwezo wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza dira, dhima na malengo yake.

## 2.6 Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika

Mfumo wa Kieletroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS) ulianza kutumika rasmi mwezi Mei, 2020 ili kuongeza ufanisi na kuimarisha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali baina ya Ofisi ya Msajili, Wizara za Kisekta, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Mfumo huo umeunganishwa na mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mfumo wa Kielekroniki wa Malipo Serikalini (GePG), ambapo unatumika kwa ajili ya usajili wa Mashirika, uwasilishaji na uhuishaji wa taarifa, pamoja na ulipaji wa ada mbalimbali.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo iliboresha Mfumo wa NIS kwa kuongeza kipengele cha Ramani ya Kidijitali ya Utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs Digital Mapping Tool), ambayo ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, tarehe 05 Oktoba, 2023 wakati wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Ramani hiyo ya kidigitali itayawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuonekana pale yanapofanyia kazi, miradi inayotekelezwa, rasilimali zilizopo na wanufaika wake, pamoja na kutoa fursa zaidi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiseriklai kutambulisha kazi zao na kuongeza wigo wa ubia na Taasisi zinazopenda kushirikiana na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na hivyo kuongeza uwazi, uwajibikaji, uendelevu na fursa mbalimbali za ufadhili kwa kutumia teknolojia rahisi.

## 2.7 Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Kwa kuzingatia kuwa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni mtambuka, Wizara imeanzisha Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Wizara za Kisekta kwa lengo la kuboresha uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Madawati hayo yalizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), tarehe 04 Oktoba, 2022 wakati wa kilele cha Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kilichofanyika Jijini Dodoma.

Waratibu wa Madawati hayo katika Wizara za Kisekta, Wasajili Wasaidizi na Viongozi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wamepewa uwezo wa kuingia kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS). Hatua inayoendelea hivi sasa ni uanzishaji wa Madawati ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi.

## 2.8 Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali lilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, tarehe 30 Septemba, 2021 jijini Dodoma kwa lengo la kuendeleza ushirikiano baina ya Serikali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo.

Aidha, Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) alikuwa Mgeni Rasmi wa Jukwaa lililofanyika tarehe 03 na 04 Oktoba, 2022; Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango alikuwa Mgeni Rasmi wa Jukwaa lililofanyika tarehe 03 hadi 05 Oktoba, 2023; na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb) alikuwa Mgeni Rasmi wa Jukwaa tarehe 04 hadi 06 Septemba, 2024.

Jukwaa la Mwaka hutanguliwa na Majukwaa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika ngazi za Wilaya na Mikoa, ambako hufanyika majadiliano ya kubadilishana uzoefu kuhusu fursa na changamoto katika utekelezaji wa shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mafunzo ya kujengeana uwezo, utambuzi wa Mashirika yaliyofanya vizuri na maazimio ya kushughulikia changamoto zilizoibuliwa na wadau mbalimbali.

## 2.9 Vikao Kazi vya Kisekta kati ya Wizara na Mashirika

Vikao Kazi vya Kisekta kati ya Wizara na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni sehemu ya utekelezaji wa Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara wa mwaka 2020, amabo unalenga kuimarisha ushirikiano baina ya Wizara yenye dhamana ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara, Idara na Taasisi za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Tayari kimefanyika kikao kazi cha kisekta cha Mashirika yanayotekeleza afua za afya kilichofanyika mkoani Dodoma mwezi Januari 2023; kikao kazi cha Mashirika yenye afua za watoto mkoani Mwanza mwezi Machi, 2023; kikao kazi cha Mashirika yenye afua za maji mkoani Morogoro mwezi Novemba, 2023; na kikao kazi cha Mashirika yenye afua za elimu mkoani Arusha tarehe 24 Novemba, 2023. Aidha, mwezi Julai 2024, kilifanyika kikao kazi cha Mashirika yenye afua za maji kilichofanyika mkoani Morogoro, ikiwa ni maandalizi ya mpango kazi wa uandaaji wa taarifa ya mchango wa wadau mbalimbali katika sekta ya maji.

## 2.10 Mahitaji ya Kisheria na Kikanuni Baada ya Usajili

Katika utekelezaji wa shughuli zake, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanapaswa kuzingatia mahitaji ya msingi ya kisheria na kikanuni kama ifuatavyo:

(a) Kuwasilisha taarifa za robo mwaka kwa mujibu Kanuni ya 20 ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 685/2019).

(b) Kuwasilisha taarifa za mwaka za utekelezaji na za fedha zilizokaguliwa kwa mujibu wa Kifungu cha 29(1)(a) na (b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya kiiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

(c) Kufanya malipo ya ada ya mwaka, usajili na taarifa za uhakiki wa Shirika kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 38(2)(b) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

(d) Kuweka wazi taarifa za vyanzo vya mapato na uwasilishaji wa mikataba ya ufadhili kwa mujibu wa Kanuni ya 13(a), (b) na (c) ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2018 (Tangazo la Serikali, 608/2018).

(e) Kuhuisha taarifa kuhusu mabadiliko mbalimbali yaliyofanyika ndani ya Shirika Lisilo la Kiserikali kwa mujibu wa Kifungu cha 33 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

(f) Kuandaa Mpango Mkakati wa Uendelevu wa Shirika, kutunza rejesta ya mali na kuweka sera za ndani za Shirika kwa mujibu wa Kanuni ya 14 ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2018 (Tangazo la Serikali, 608/2018).

## 2.11 Uwasilishaji wa Taarifa na Ulipaji wa Ada

Kwa mwaka 2023, jumla ya Mashirika Yasiyo a Kiserikali 1,368 yaliwasilisha taarifa za utekelezaji na taarifa za fedha zilizokaguliwa kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 7,931 yaliyopaswa kuwasilisha taarifa hizo. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 17 ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyopaswa kuwasilisha taarifa za mwaka 2023.

Aidha, idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyowasilisha taarifa imeongezeka kutoka 1,257 mwaka 2022 hadi 1,368 (Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kitaifa 1,021, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa 258, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimkoa 42 na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kiwilaya 47) kwa mwaka 2023, ikiwa ni ongezeko la asilimia 32. Jedwali 2.11.1 na Jedwali 2.11.2 limefafanua zaidi kuhusu idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyowasilisha taarifa kwa ngazi ya usajili na kimkoa kama inayoonekana hapo chini:

*Jedwali 2.11.1: Mashirika Yaliyowasilisha Taarifa kwa Ngazi ya Usajili*

| Na | Ngazi ya Usajili | Idadi |
|---|---|---|
| 01 | Kimataifa | 258 |
| 02 | Kitaifa | 1021 |
| 03 | Kimkoa | 42 |
| 04 | Kiwilaya | 47 |
| | **Jumla** | **1,368** |

*Jedwali 2.11.2: Mashirika Yaliyowasilisha Taarifa kwa Ngazi ya Mkoa*

| Na | Mkoa | Idadi |
|---|---|---|
| 01 | Arusha | 239 |
| 02 | Dar es Salaam | 436 |
| 03 | Dodoma | 51 |
| 04 | Geita | 9 |
| 05 | Iringa | 40 |
| 06 | Kagera | 36 |
| 07 | Katavi | 4 |
| 08 | Kigoma | 24 |
| 09 | Kilimanjaro | 64 |
| 10 | Lindi | 13 |
| 11 | Manyara | 18 |
| 12 | Mara | 23 |
| 13 | Mbeya | 44 |
| 14 | Morogoro | 46 |
| 15 | Mtwara | 24 |
| 16 | Mwanza | 115 |
| 17 | Njombe | 21 |
| 18 | Pwani | 32 |
| 19 | Rukwa | 23 |
| 20 | Ruvuma | 16 |
| 21 | Shinyanga | 19 |
| 22 | Simiyu | 6 |
| 23 | Singida | 10 |
| 24 | Songwe | 8 |
| 25 | Tabora | 15 |
| 26 | Tanga | 32 |
| | **Total** | **1,368** |

Vilevile, jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 3,297 yamelipa ada za mwaka 2023 kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 7,931 yaliyotakiwa kulipa ada katika kipindi husika, ikiwa ni sawa na asilimia 42. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalifanya malipo ya ada ya mwaka, lakini hayakuwasilisha taarifa.

Kwa kiasi kikubwa, hali hiyo inapunguza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa. Jedwali 2.11.3 na Jedwali 2.11.4 limefafanua zaidi kuhusu idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyolipa ada kwa ngazi ya usajili na kimkoa kama inavyoonekana hapo chini:

*Jedwali 2.11.3: Mashirika Yaliyolipa Ada kwa Ngazi ya Usajili*

| Na | Ngazi ya Usajili | Idadi |
|---|---|---|
| 01 | Kimataifa | 405 |
| 02 | Kitaifa | 2,624 |
| 03 | Kimkoa | 105 |
| 04 | Kiwilaya | 163 |
| | **Jumla** | **3,297** |

*Jedwali 2.11.4: Mashirika Yaliyolipa Ada kwa Ngazi ya Mkoa*


| Na | Mkoa | Idadi |
|---|---|---|
| 01 | Arusha | 581 |
| 02 | Dar es Salaam | 1,052 |
| 03 | Dodoma | 115 |
| 04 | Geita | 23 |
| 05 | Iringa | 84 |
| 06 | Kagera | 87 |
| 07 | Katavi | 12 |
| 08 | Kigoma | 72 |
| 09 | Kilimanjaro | 167 |
| 10 | Lindi | 25 |
| 11 | Manyara | 45 |
| 12 | Mara | 66 |
| 13 | Mbeya | 98 |
| 14 | Morogoro | 134 |
| 15 | Mtwara | 46 |
| 16 | Njombe | 51 |
| 17 | Pwani | 88 |
| 18 | Rukwa | 37 |
| 19 | Ruvuma | 41 |
| 20 | Shinyanga | 41 |
| 21 | Singida | 34 |
| 22 | Songwe | 16 |
| 23 | Tabora | 40 |
| 24 | Tanga | 94 |
| | **Jumla** | **3,297** |

Aidha, kwa mwaka 2023, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 188 yaliwasilisha mikataba au hati za makubaliano ya ufadhili wa miradi kwa mujibu wa Kanuni ya 13(a) ya Marekebisho ya Kanuni za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za mwaka 2018 (Tangazo la Serikali, 608/2018). Jumla ya mikataba 500 yenye kiasi cha shilingi 671,674,824,465 iliwasilishwa, kufanyiwa uchambuzi na kuidhinishiwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali 2.11.5:

*Jedwali 2.11.5: Mikataba Iliyowasilishwa na Kuidhinishwa*

| Na | Sekta/Afua | Idadi ya Mikataba | Kiasi cha Fedha |
|---|---|---|---|
| 01 | Afya | 80 | TZS 315,974,139,953/- |
| 02 | Uwezeshaji wa Jamii Kiuchumi | 150 | TZS 119,679,172,974/- |
| 03 | Ulinzi wa Jamii | 51 | TZS 64,816,673,711/- |
| 04 | Elimu | 60 | TZS 53,793,732,373/- |
| 05 | Kilimo | 32 | TZS 41,968,001,880/- |
| 06 | Mazingira | 54 | TZS 29,061,765,868/- |
| 07 | Utawala Bora | 29 | TZS 25,652,229,467/- |
| 08 | Haki za Binadamu | 15 | TZS 5,625,643,553/- |
| 09 | Jinsia | 17 | TZS 5,245,312,011/- |
| 10 | Nishati | 3 | TZS 5,245,312,011/- |
| 11 | Maji | 9 | TZS 4,232,509,122/- |
| | **JUMLA** | **500** | **TZS 671,674,824,465/-** |

*Umbo 2.11.5: Mikataba Iliyowasilishwa na Kuidhinishwa*



## 2.12 Uzoefu wa Nchi Nyingine katika Uratibu wa Mashirika

Uzoefu wa nchini nyingine kupitia ziara za kujifunza na vyanzo vya wazi vya taarifa unaonesha kuwa mifumo ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika baadhi ya nchi inafanana kwa kiasi kikubwa, ambapo jukumu la usajili na uratibu lipo chini ya Bodi za Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali za nchi husika. Vilevile, imebainika kuwa vigezo na taratibu za usajili, pamoja na mahitaji ya kisheria baada ya usajili yanafanana kwa kiasi kikubwa na hali ya hapa nchini.

Kama ilivyo hapa nchini, mahitaji usajili wa Shirika Lisilo la Kiserikali kupitia Bodi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikal nchini Kenya (Non-Governmental Organizations Coordination Board) na Bodi ya Utawala nchini Rwanda (Rwanda Governance Board – RGB) ni pamoja na nakala za katiba, mihtasari ya vikao vya wanachama, wasifu na picha za viongozi, barua za utambulisho na ada ya usajili. Vilevile, baada ya kukamilika kwa mchakato wa usajili, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hutakiwa kufanya malipo ya ada ya mwaka, kuwasilisha taarifa za mwaka za utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali, mpango kazi na bajeti, pamoja na uthibitisho wa ufadhili.

Aidha, masuala ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanafanywa kwa ushirikiano kati ya Bodi za Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mabaraza ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Kadhalika, Bodi za Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zipo ama chini ya Wizara za Mambo ya Ndani ya Nchi au Wizara za Maendeleo ya Jamii.

Mathalani, nchini Malawi, usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unafanywa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (Non-Governmental Organizations Regulatory Authority – NGORA) ambayo ipo chini ya Wizara ya Jinsia, Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii na kwamba lipo pia Baraza la la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (Council for Non-Governmental Organizations in Malawi – CONGOMA). Wakati NGORA imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2022, CONGOMA imeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 24 na 25 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2000.

Kwa upande mwingine, usajili na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini Uganda unafanywa na Taasisi ya Kitaifa ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (National Bureau for NGOs), ambayo ipo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kwamba lipo Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Nchini Uganda (Uganda NGOs Forum – UNNGOF).

Hata hivyo, Jukwaa la Kitaifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Nchini Uganda (UNNGOF) halijaanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge kama ilivyo kwa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (National Council of NGOs – NaCoNGO), ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 25 cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

# SURA YA TATU

## Mapato, Matumizi na Mikakati Mbalimbali ya Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

### 3.1 Utangulizi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 29 (1) (a) na (b) ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuwasilisha taarifa za mwaka za utekelezaji na taarifa za fedha zilizokaguliwa. Kupitia uchambuzi wa taarifa hizo, Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali inaweza kubainisha kiwango cha fedha kilichopokelewa na kutumiwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mwaka husika, pamoja na mikakati mbalimbali ya uendelevu wa Mashirika hayo.

### 3.2 Mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali


Uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,368 yaliyowasilisha taarifa ake kwa ukamilifu yalipata fedha kiasi cha Shilingi **2,614,880,491,980** kutoka katika vyanzo mbalimbali vya fedha. Kiasi hicho ni ongezeko la Shilingi **365,635,645,700** ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 14 ya mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikilinganishwa na kiasi cha fedha kilichopokelewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali mwaka 2022.

Aidha, kiasi hicho cha mapato ya fedha za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2023 ni sawa na asilimia 06 ya Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2023/2024. Mchanganuo wa vyanzo vya mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2023 yameainishwa kwenye Jedwali 3.2 na Umbo 3.2 hapo chini:

## *Jedwali 3.2: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika*

| Na | Vyanzo vya Mapato | Kiasi cha Fedha |
|---|---|---|
| 01 | Bakaa | TZS 37,925,158,488/- |
| 02 | Msamaha wa Kodi | TZS 271,659,205/- |
| 03 | Ruzuku | TZS 3,281,674,634/- |
| 04 | Michango ya Wanachama | TZS 7,013,683,724/- |
| 05 | Mapato ya Vitega Uchumi | TZS 8,355,014,956/- |
| 06 | Malipo ya Huduma | TZS 6,954,741,585/- |
| 07 | Michango ya Jamii | TZS 3,575,676,963/- |
| 08 | Wafadhili wa Ndani | TZS 29,939,831,796/- |
| 09 | Michango kutoka Sekta Binafsi | TZS 7,130,106,831/- |
| 10 | Wafadhili wa Nje | TZS 2,510,432,943,798/- |
| | **Jumla** | **TZS 2,614,880,491,980/-** |

## *Umbo 3.2: Vyanzo vya Mapato ya Mashirika*



Taarifa hii ya mapato inaonesha kuwa, asilimia 96.01 ya mapato ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanategemea fedha kutoka kwa wafadhili wa nje. Aidha, michango ya wafadhili wa ndani katika utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali za kusaidia jamii kwa mwaka 2023 imeongezeka kwa kiasi cha Shilingi 11,163,209,910, ambayo ni sawa na asilimia 37.29. Hata hivyo, nguvu zaidi inatakiwa kuelekezwa kwenye eneo la mapato ya vitega uchumi, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ambao utayawezesha Yasiyo ya Kiserikali kuwa na vyanzo vya kudumu vya mapato.


## 3.3 Matumizi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yalitumia kiasi cha Shilingi **2,461,926,876,419** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi pamoja na malipo ya posho na mishahara, pamoja na kodi mbalimbali za Serikali kama ilivyoainishwa katika Jedwali 3.3 na Umbo 3.3 hapo chini:

*Jedwali 3.3: Matumizi ya Fedha za Mashirika*

| Na | Aina ya Matumizi | Kiasi cha Fedha |
|---|---|---|
| 01 | Miradi | TZS 2,139,495,506,090/- |
| 02 | Posho na Mishahara | TZS 245,004,730,237/- |
| 03 | Kodi ya Ujuzi (SDL) | TZS 2,814,636,314/- |
| 04 | Kodi ya Mishahara (PAYE) | TZS 42,598.958,274/- |
| 05 | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) | TZS 30,858,702,827/- |
| 06 | Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) | TZS 1,154,342,677/- |
| | **Jumla** | **TZS 2,461,926,876,419/-** |

*Umbo 3.3 Matumizi ya Fedha za Mashirika*




Uchambuzi wa matumizi ya fedha zilizopokelewa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2023 unaonesha kuwa asilimia 87 ya fedha zilizopokelewa ilitumika katika utekelezaji wa miradi, asilimia 10 ulipaji wa posho na mishahara na asilimia 0.10 ilitumika katika ulipaji wa tozo na kodi mbalimbali za Serikali, ikiwemo SDL, NSSF, PAYE na WCF

## 3.4 Mikakati ya Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Kupitia uchambuzi wa taarifa za mwaka, taarifa za robo mwaka, taarifa za mikataba ya ufadhili zilizowasilishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Njombe, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Singida, Tabora na Tanga, imebainika kuwa idadi kubwa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali bado imeendelea kutegemea zaidi fedha za ufadhili kutoka kwa wahisani.

Hata hivyo, baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamebainika kuanza kubuni mbinu mbalimbali kwa ajili ya kuhakikisha miradi yao inakuwa na uendelevu. Mathalani, Shirika la Tanzania Early Childhood Education and Care (TECEC) linamiliki kituo cha mafunzo ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, pamoja na mashine ya kusaga unga wa lishe katika eneo la Nyamalango – Nyegezi Jijini Mwanza.

Shirika la TECEC pia linatengeneza zana za kujifunzia kwa kutumia malighafi zisizo na gharama, ikiwemo vipande vya maboksi.

Aidha, Shirika la Tanzania People Development Organization (TADEPO) limewezesha ukarabati wa jengo moja na ujenzi wa jengo la upasuaji katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga – Bombo. Vilevile, Shirika la Project Watu Kamili linamiliki kituo cha mafunzo ya ufundi stadi (ushonaji na ususi) kwa vijana walio katika mazingira hatarishi Mkoani Kilimanjaro, kama njia mojawapo ya kuwapatia kipato vijana rika na kuimarisha uendelevu wa miradi husika.

Kadhalika, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Gabriella Children's Rehabilitation Centre, Organization of Youth Against Risk Behaviors (OYARB), Courage on Recovery Foundation (CRF) na Youth Empowerment and Pyschotherapy Aid Organization (YEPAO), yamekuwa yakipokea michango ya rasilimali fedha na vifaa kutoka kwa wazazi na walezi wa watoto wenye mahitaji maalum wanaohudumiwa na Shirika la Gabriella na warahibu za dawa za kulevya wanaohudumiwa na Mashirika ya OYARB, CRF na YEPAO Mkoani Kilimanjaro ili kuhakikisha uendelevu wa miradi inayotekelezwa.




*Pichani ni Jengo la Shirika la Tumaini Jipya la Wanawake Kilwa **(TUJIWAKI)** ambalo ndani yake kuna Ofisi, ukumbi wa mikutano na chumba cha biashara. Ujenzi wa Jengo hilo umefadhiliwa na Shirika la ActionAid Tanzania kama mkakati wa kuhakikisha uendelevu wa Shirika la **TUJIWAKI.***

# SURA YA NNE

## Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Katika Nyanja Mbalimbali za Maendeleo

### 4.1 Utangulizi

Kama ilivyoelezwa kwenye Sura ya Kwanza ya taarifa hii, mwaka 2001, Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuweka mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi na kijamii. Aidha, Sera hiyo imeweka misingi thabiti ya utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali za maendeleo na Taifa kwa ujumla kupitia utekelezaji wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania na Kanuni zake.

Katika utekelezaji wa shughuli zake, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Malengo, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, ikiwemo Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996), Sera ya Taifa ya Maji (2002), Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii (2003), Sera ya Afya (2007), Sera ya Taifa ya Kilimo (2013), Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013), Sera ya Elimu na Mafunzo (2014), Sera ya Taifa ya Mazingira (2021), Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023), Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030).

### 4.2 Utekelezaji wa Miradi na Afua Kisekta

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,368 yalikuwa yamepokea kiasi cha shilingi 2,139,507,191,396 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali, pamoja na masuala ya kiutawala. Mathalani, taarifa zinaonesha kuwa kiasi cha shilingi 930,568,771,806 kilitumika katika shughuli za kiutawala, ilhali kiasi cha shilingi 1,208,938,419,590 kilitumika kutekeleza miradi takribani 2,643 hususani katika sekta ya afya, uwezeshaji wa jamii kiuchumi, ulinzi wa jamii, mazingira, elimu, kilimo, utawala bora, maji, haki za binadamu, jinsia, nishati na miundombinu.



*Pichani ni baadhi ya mitambo ya mradi wa kufua umeme wa maji unaomilikiwa na kutekelezwa na Shirika la CEFA - International Committee for Agriculture Training and Cooperation katika Kijiji cha Ikondo, Kata ya Lupembe, Wilaya ya Njombe Mkoani Njombe.*

## *Jedwali 4.2: Mchanganuo wa Fedha Kisekta*

| Na | Sekta/Afua | Kiasi cha Fedha |
|---|---|---|
| 01 | Afya | TZS 507,017,325,261/- |
| 02 | Uwezeshaji wa Jamii Kiuchumi | TZS 281,384,110,075/- |
| 03 | Ulinzi wa Jamii | TZS 122,489,218,811/- |
| 04 | Mazingira | TZS 98,690,465,665/- |
| 05 | Elimu | TZS 79,166,785,015/- |
| 06 | Kilimo | TZS 47,977,264,569/- |
| 07 | Utawala Bora | TZS 36,287,582,890/- |
| 08 | Maji | TZS 12,846,489,968/- |
| 09 | Jinsia | TZS 11,505,579,244/- |
| 10 | Haki za Binadamu | TZS 10,343,174,647/- |
| 11 | Nishati | TZS 772,541,413/- |
| 12 | Miundombinu | TZS 457,882,032/- |
| | **Jumla** | **TZS 1,208,938,419,590/-** |

## 4.2.1 Sekta ya Afya

Kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Afya ya mwaka 2007, sekta ya afya ni muhimu kwa maendeleo ya watu. Sekta hii inajumuisha miundombinu, wataalamu, vifaa na vifaa tiba, vitendanishi, dawa, tiba, kinga na bima ya afya. Vilevile, sehemu ya 5.5.2 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine unalenga kuimarisha mifumo ya usimamizi, upatikanaji na utoaji wa huduma za afya, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya na uhamasishaji wa matumizi ya bima ya afya.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2023 sekta ya afya ilitumia kiasi cha Shilingi 507,017,325,261 kutekeleza miradi na afua za kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya, kuzuia maambukizi ya VVU/UKIMWI (HIV/AIDS), afya ya jamii, lishe, matibabu ya macho, fistula, kansa, kifua kikuu, tohara, utoaji wa viungo bandia, afya ya uzazi, maendeleo ya awali ya mtoto, afya ya mama na mtoto, elimu ya afya ya uzazi kwa vijana balehe, vifaa tiba na chanjo.
Aidha, washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR), Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Tanzania (CDC-Tanzania), Mfuko wa Global Fund, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (FCDO), Shirika la Bill and Melinda Gates Foundation, Shirika la Amref Health Africa, Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika (CDC-Africa) na Taasisi ya Master Card Foundation.

Aidha, washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR), Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Tanzania (CDC-Tanzania), Mfuko wa Global Fund, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (FCDO), Shirika la Bill and Melinda Gates Foundation, Shirika la Amref Health Africa, Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika (CDC-Africa) na Taasisi ya Master Card Foundation.

## 4.2.2 Uwezeshaji wa Jamii Kiuchumi

Sambamba na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), sehemu ya 2.5.3 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine imejielekeza kuimarisha uwezeshaji jamii na mipango ya maendeleo ya sekta binafsi; kuhamasisha ushirikishwaji na uwezeshaji kiuchumi kwa watu wenye ulemavu na tabia ya kuweka akiba na kuwekeza katika shughuli za uzalishaji; pamoja na kuimarisha usimamizi wa mifuko ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Kwa kuzingatia kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni moja ya wadau muhimu katika kuiwezesha jamii na kuimarisha uwezo wao wa kujitegemea, katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sekta ya uwezeshaji wa jamii kiuchumi ilitumia kiasi cha Shilingi 281,384,110,075 kutekeleza miradi iliyolenga kuwafikia watoto wenye usonji, kutoa bima ya afya kwa watoto, uwezeshaji wa masuala ya haki na usawa wa kijinsia, pamoja na kusaidia watoto yatima.

Miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa vikundi vya vijana na wanawake kuhusu fursa mbalimbali za kiuchumi ikiwemo mikopo ya Halmashauri (4/4/2), uwezeshaki katika afua za kilimo na maji, biashara na uwekezaji, kuwajengea uwezo vijana kwenye masuala ya uongozi na elimu ya uraia, kuwasaidia wanawake wajane, uzalishaji na uongezaji thamani kwenye bidhaa na mazao ya kilimo, fursa za ajira kwa vijana, pamoja na uwezeshaji wa watu wenye mahitaji maalum.

Aidha, washirika wa maendeleo walioongoza kufadhili miradi na afua za uwezeshaji wa jamii kiuchumi ni pamoja na Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Taasisi ya Master Card Foundation, Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD), Shirika la Bill and Melinda Gates Foundation, Shirika la World Family of Radio Maria Onlus, Shirika la ACN International and Voce Di Maria, Ubalozi wa Sweden, Ubalozi wa Ireland, Benki Kuu ya Tanzania (BOT), na Taasisi ya Global Affairs Canada (GAC).



*Pichani ni wanachama wa kikundi cha kuweka na kukopa cha Tunaweza Group kilichopo katika Kata ya Mtipa, Manispaa ya Singida Mkoani Singida. Kikundi hicho kimewezeshwa na Shirika la Brac Maendeleo Tanzania.*

## 4.2.3 Ulinzi wa Jamii

Sehemu ya 5.5.6 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine imejielekeza kuimarisha huduma za malezi mbadala ikiwemo malezi ya kambo na kuasili watoto, juhudi za kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto; huduma za malezi, makuzi, maendeleo ya awali ya mtoto; utoaji wa huduma za ustawi wa Jamii ikiwemo huduma za afya, unasihi na msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa makundi yenye uhitaji katika jamii; pamoja na upatikanaji wa huduma za msingi kwa wazee.

Kwa msingi huo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakitoa mchango mkubwa katika jitihada za pamoja za kuanzisha na kuhamasisha jamii kupitia programu mbalimbali za ulinzi wa jamii hususani za kulinda maslahi na ustawi wa watoto, wazee, wajane, wanawake, vijana, watu wenye ulemavu na watoto yatima hususani kupitia utekelezaji wa miradi ya uendeshaji wa makao ya watoto, huduma malezi ya awali kwa watoto, nyumba salama na vituo vya kulelea watoto wadogo mchana.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sekta ya ulinzi wa jamii ilitumia kiasi cha Shilingi 122,489,218,811 kutekeleza miradi na afua za elimu kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kuweka mazingira salama kwa watu wenye mahitaji maalum wanaoishi katika kambi za wakimbizi, kutoa huduma ya maji, afya na lishe, kusaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuwaunganisha na familia zao, pamoja na kuzijengea uwezo familia zinazoishi katika mazingira hatarishi.

Aidha, washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kukabiliana na UKIMWI (PEPFAR), Shirika la Danish Refugee Council (DRC), Taasisi ya Rahma International Society, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), Shirika la Compassion International Inc, Shirika la Railway Children, Shirika la Givewell Foundation na Serikali ya Ujerumani (BMZ) kupitia Idara ya Mambo ya Nje (GFFO).




*Pichani ni watoto wakiwa katika Kituo cha Awali cha Malezi na Makuzi katika Kata ya Uswitu, Wilaya ya Nzega Mkoani Tabora. Kituo hicho kimeanzishwa kwa ufadhili wa Shirika la Brac Maendeleo Tanzania.*

## 4.2.4 Uhifadhi wa Mazingira

Kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Mazingira (2021), mazingira na maliasili asilia ni tunu ya Taifa na msingi wa maendeleo endelevu. Kwa msingi huo, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi, imeendelea kuimarisha mifumo mbalimbali ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira, pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali asilia kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo.

Vilevile, sehemu ya 5.3.5 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine umejielekeza kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu; kupunguza uchafuzi wa mazingira pamoja na athari zake; kuimarisha uwezo wa Taifa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; kupunguza uharibifu wa ardhi; kuboresha upandaji wa miti kibiashara; na kuendeleza mikakati ya kupambana na ujangili, biashara haramu na uvunaji haramu wa rasilimali za wanyamapori na misitu.

Kwa kuzingatia kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni washiriki muhimu katika ulinzi, uhifadhi na utunzaji wa Mazingira, katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sekta ya uhifadhi wa mazingira ilitumia kiasi cha Shilingi 98,690,465,665 kutekeleza miradi iliyolenga kuwezesha mamlaka za uhifadhi katika kuboresha hifadhi za Taifa, kuweka mazingira rafiki na jamii zinazozunguka hifadhi, upandaji miti na uhifadhi wa misitu, utunzaji wa vyanzo vya maji, uhifadhi wa mazingira, upandaji wa miti mashuleni, miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, kujengea uwezo jamii katika utunzaji wa mazingira, uhifadhi wa ndege na wanyamapori, pamoja na uhifadhi wa fukwe za bahari, mito na maziwa.

Aidha, washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili ni pamoja na Shirika la Jane Goodhall Institute, Shirika la Misaada la Marekani USAID, Shirika la Maendeleo la Norway (NORAD), Shirika la African Wildlife Foundation (AWF), Shirika la World Wide Fund for Nature Sweden (WWF Sweden), Shirika la World Wide Fund for Nature UK (WWF UK), Shirika la World Wide Fund for Nature Germany (WWF Germany), Shirika la Solidaridad Eastearn and Central Africa Expertise Centre (ECA-Tanzania), Shirika la The Nature Conservancy, pamoja na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA).



*Pichani ni Maafisa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, pamoja na Wizara ya Fedha, wakipata maelezo kuhusu vitalu vya miche ya miti ya kisasa na ya asili vinavyozalishwa na Shirika la Forest Focus katika Wilaya Korogwe Mkoani Tanga*




*Pichani juu ni baadhi ya majengo ya madarasa na vyoo katika Shule ya Msingi Eternal inayomilikiwa na Shirika la Eternal Families Tanzania Mkoani Tabora. Pichani chini ni baadhi ya wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi Eternal.*



*Pichani ni mradi wa vyumba kumi (matundu 10) ya vyoo vya wanafunzi katika Shule ya Msingi Kitupa katika Wilaya ya Mpimbwe Mkoani Katavi. Mradi huu umefadhiliwa na Shirika la ActionAid Tanzania.*

## 4.2.5 Sekta ya Kilimo

Kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Kilimo (2013), uchumi wa Tanzania umeendelea kutegemea zaidi kilimo, licha ya mchango wake katika Pato la Taifa kuendelea kushuka. Sekta ya Kilimo imeendelea kuwa kitovu cha ukuzaji wa viwanda na maisha ya watu nchini, ambapo inakadiriwa kuwa kinaajiri takribani asilimia 66.3 ya nguvukazi, ambapo wanawake ni asilimia 52 na wanaume asilimia 48.

Aidha, sehemu ya 5.3.1 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, imejielekeza kufungamanisha sekta ya kilimo na sekta nyingine za kiuchumi, kujenga mazingira mazuri kwa sekta binafsi kuendesha shughuli za uzalishaji na kuendelea kuimarisha programu za mafunzo. Hatua hizi, zinalenga kuongeza thamani na tija ya uzalishaji wa mazao ya kilimo, kuzalisha ajira, kutanua wigo mseto wa bidhaa na kuimarisha mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sekta ya kilimo ilitumia kiasi cha Shilingi 47,977,264,569 kutekeleza miradi ya kuwajengea uwezo wakulima na Maafisa Ugani kuhusu uzalishaji bora na mbegu za kilimo, elimu kwa wanawake kutumia mbinu za asili katika kilimo, kuwajengea uwezo vijana katika masuala ya kilimo, ufugaji wa kuku, kilimo cha mironge na zabibu, kufanya tafiti, kuhamasisha kilimo endelevu cha kahawa, usambazaji wa pembejeo za kilimo, kuongeza thamani kwenye mazao, pamoja na upatikanaji wa masoko ya bidhaa za kilimo.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa, washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili katika sekta ya kilimo ni pamoja na Shirika la VI Agro Forestry, Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Bill and Melinda Gates Foundation, Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Shirika la Bread for the World, Shirika la Maendeleo, Ushirikiano na Misaada ya Kibinadamu la Ubelgiji (Directorate General for Development Cooperative and Humanitarian Aid - DGD), Shirika la Care International (USA), Taasisi ya Global Affairs Canada (GAC), Serikali ya Sweden, pamoja na Taasisi ya Royal Norwegian Society for Development (Norges Vel).



*Pichani ni Maafisa kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wafanyakazi wa Shirika la Brac Maendeleo Tanzania wakiwa na mnufaika wa mradi wa kilimo cha mbogamboga katika Kata ya Wamaku, Wilaya ya Singida Mkoani Singida.*

### 4.2.6 Utawala Bora

Mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki ni muhimu katika kuimarisha usawa na ustawi wa jamii. Utoaji na upatikanaji wa haki unawezekana ikiwa kuna mifumo imara ya kitaasisi. Mifumo hiyo inajumuisha watumishi wenye weledi, vitendea kazi, miundombinu wezeshi na miongozo rafiki katika utoaji haki. Kwa msingi huo, mifumo ya utoaji na upatikanaji wa haki ni moja ya nguzo muhimu za utawala bora.

Vilevile, sehemu ya 5.5.8 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine imejielekeza kuboresha mifumo na miundombinu ya utoaji wa haki, kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji na upatikanaji wa haki, pamoja na kuimarisha taratibu na miongozo ya utoaji wa msaada wa kisheria nchini. Aidha, baadhi ya malengo ya kimkakati ya Mpango Mkakati wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wa Mwaka 2023-2026 ni pamoja na kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kuzuia rushwa na kuimarisha uzingatiaji wa misingi ya utawala bora.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sekta ya utawala bora ilitumia kiasi cha Shilingi 36,287,582,890 kutekeleza miradi ya kuwajengea uwezo vijana na wanawake kuhusu masuala ya uongozi, haki za kiuchumi, mafunzo kuhusu elimu ya uraia, kushawishi mabadiliko ya sera, utekelezaji wa programu na mikakati ya kukuza utawala bora, kuhimiza masuala ya sheria, haki za binadamu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji; usaidizi wa masuala ya kisheria kwa makundi mbalimbali.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa washirika wa maendeleo walioongoza kwa ufadhili katika sekta ya utawala bora ni pamoja na Ubalozi wa Sweden, Ubalozi wa Norway, Taasisi ya Hempel Foundation, Shirika la Konrad-Adenauer-Stiftung, Shirika la Misaada la Marekani (USAID), pamoja na Shirika la Freedom House Inc.

### 4.2.7 Sekta ya Maji

Kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Taifa ya Maji (2002), huduma ya maji ni sehemu ya mahitaji muhimu yanayochochea maendeleo ya watu. Sekta hii inahusisha upatikanaji na usambazaji wa maji pamoja na utunzaji wa vyanzo vya maji. Vilevile, mpango wa maendeleo na usimamizi wa usambazaji wa maji vijijini na mijini unahitaji mahusiano ya kitaasisi miongoni mwa wadau muhimu ambao ni Serikali, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na jamii kwa ujumla.

Aidha, sehemu ya 5.5.3 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine, imetoa kipaumbele katika upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama vijijini na mijini, utunzaji wa vyanzo vya maji; uimarishaji wa miundombinu jumuishi ya upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama mijini na vijijini, pamoja na uimarishaji wa programu za uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sekta ya maji ilitumia kiasi cha Shilingi 12,846,489,968 kutekeleza miradi na afua mbalimbali katika masuala ya elimu ya afya na usafi wa mazingira mashuleni na kwenye jamii, uchimbaji wa visima vya maji vijijini na mijini, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya maji, mafunzo kwa kamati za maji vijijini kuhusu utunzaji wa miundombinu ya maji na uhifadhi wa vyanzo vya maji, pamoja na uboreshaji wa huduma za maji.

Aidha, washirika wa maendeleo walioongoza katika ufadhili wa sekta ya maji ni pamoja na Shirika la Charity Water, Mfuko wa Kuhudumia Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF), Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW), Shirika la Water for People (USA), Shirika la Life Water International, Shirika la WF-AID (UK), Shirika la Catholic Relief Services, Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza (FCDO), Umoja wa Ulaya (EU), pamoja na Taasisi ya Go Drill Inc.



*Pichani ni mradi wa maji katika Shule ya Msingi Msanga iliyopo katika Wilaya ya Chamwino Mkoani Dodoma. Mradi huu umefadhiliwa na Shirika la ActionAid Tanzania kupitia Mpango wa Ufadhili wa Mtoto*

## 4.2.8 Masuala ya Kijinsia

Ushiriki wa wanawake katika nyanja mbalimbali ni muhimu ili kuleta usawa na kuondoa ukatili wa kijinsia. Ni kwa msingi huo, sehemu ya 2.5.3 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine imejielekeza katika utekelezaji wa miradi na afua zenye lengo la kuleta usawa wa kijinsia kwa wanawake na wasichana, kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa wasichana, hatua za haraka dhidi ya ubaguzi katika masuala ya umiliki wa ardhi na urithi, unyanyasaji dhidi ya wanawake, pamoja na kuongeza elimu dhidi ya mila na tamaduni zinazomkandamiza mwanamke.

Aidha, kwa mujibu wa sehemu ya 5.2.26 ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake (2023), Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana wajibu wa kuingiza masuala ya kijinsia katika mipango, programu na mikakati yao, kukuza na kutetea haki za wanawake, wanaume, wasichana na wavulana, kuhamasisha ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika ngazi mbalimbali za maamuzi, kuhamasisha utengaji wa bajeti kwa ajili ya mahitaji ya makundi maalum katika jamii hususan watu wenye ulemavu, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na watu wanaoishi na VVU/UKIMWI, pamoja na kutekeleza programu za kuhamasisha usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sekta ya jinsia ilitumia kiasi cha Shilingi 11,505,579,244 kutekeleza miradi katika kuhamasisha masuala ya usawa wa kijinsia, kuwajengea uwezo wasichana na wanawake kuhusu haki zao za msingi, masuala ya uongozi na utawala bora, nyumba salama, elimu na kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia na kwa watoto, fursa mbalimbali za uongozi kwa wanawake, kuwawezesha wanawake kijamii na kiuchumi, kuwezesha watoto wa kike kubaki shuleni, sambamba na kuwaelimisha na kuwezesha watoto wa kike katika masuala ya hedhi salama.

Aidha, uchambuzi unaonesha washirika wa maendeleo walioongoza katika ufadhili wa miradi ni pamoja na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Idadi ya Watu (UNFPA), Taasisi ya Global Affairs Canada (GAC), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Sweden (SIDA), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Shirika la Foundation of Civil Society (FCS) na Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake (UN – Women).

### 4.2.9 Haki za Binadamu

Kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu (2013), sehemu ya 5.5.8 ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26, pamoja na mambo mengine imejielekeza kuimarisha upatikanaji wa haki na ulinzi wa haki za binadamu nchini, pamoja na kuimarisha miongozo na taratibu za utoaji wa huduma ya misaada ya kisheria kwa wananchi.

Aidha, malengo ya kimkakati ya Mpango Mkakati wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora wa Mwaka 2023-2026 yamejikita kuimarisha afua za kukabiliana na VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza, kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kuzuia rushwa, pamoja na kuimarisha ulinzi wa haki za binadamu.

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, sekta ya haki za binadamu ilitumia kiasi cha Shilingi 10,343,174,647 kutekeleza miradi ya utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi, kuwajengea uwezo vijana, kampeni za kupinga ukatili wa kijinsia, kuwajengea uwezo na kutoa mafunzo ya kiuchumi na kisheria kwa makundi mbalimbali, uhamasishaji wa kulinda amani, utoaji wa haki za kijamii na kiuchumi kwa wanawake na wasiojiweza, kujenga uwezo kwa taasisi zinazotoa huduma ya msaada wa kisheria kwa jamii, pamoja na kutoa elimu ya utetezi na ushawishi kuhusu masuala ya haki za binadamu.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa washirika wa maendeleo walioongoza katika ufadhili ni pamoja na Shirika la T-Marc Tanzania, Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Shirika la Bread for the world, Umoja wa Ulaya (EU), Shirika la Change Africa Trust, Shirika la Protection International Africa, Shirika la Well Spring Fund, Shirika la Open Society Policy Centre (OSPC) na Shrika la Global Fund for Women.

## 4.3 Wanufaika wa Miradi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali


Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, miradi na afua ziilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imenufaisha makundi mbalimbali katika jamii. Uchambuzi unaonesha kuwa makundi yaliyoongoza kwa kufikiwa zaidi na miradi au afua zilizotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni wanawake ambao walifikiwa kwa takribani asilimia 47.4 na vijana ambao walifikiwa kwa takribani asilimia 30.5.

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa kundi la wagane ndilo lililofikiwa kwa uchache zaidi na miradi iliyotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika kipindi husika. Vievile, jumla ya taasisi 4,089,773 zikiwemo Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi zilifikiwa katika kipindi husika kama inayooneshwa kwenye Jedwali 4.3 na Umbo 4.3 hapo chini:

*Jedwali 4.3: Idadi ya Waliofikiwa na Miradi*

| Na | Waliofikiwa kwa Makundi | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 01 | Wanawake | 132,051,603 | 47.3863% |
| 02 | Watoto | 15,104,483 | 5.4202% |
| 03 | Wanaume | 42,157,323 | 15.1280% |
| 04 | Wazee | 319,993 | 0.1148% |
| 05 | Wajane | 4,611 | 0.0017% |
| 06 | Vijana | 84,915,373 | 30.4716% |
| 07 | Watu wenye Ulemavu | 26,159 | 0.0094% |
| 08 | Taasisi | 4,089,773 | 1.4676% |
| 09 | Wajane | 865 | 0.0003% |
| | **Jumla ya Waliofikiwa** | **278,670,183** | **100%** |

*Umbo 4.3: Asilimia ya Waliofikiwa na Miradi*





## 4.4 Ajira Zilizozalishwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

Uchambuzi unaonesha kuwa katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 910 yalizalisha jumla ya ajira 21,701, ambapo kati ya hizo 13,375 (Watanzania 13,256 na wageni 119) zilikuwa ajira rasmi na 8,326 (Watanzania 7,888 na wageni 438) zilizkuwa ajira za kujitolewa. Kati ya ajira hizo jumla ya ajira 11,953 zilikuwa za wanawake na 9,748 zilikuwa za wanaume. Aidha, jumla ya Shilingi 245,004,730,237 zilitumika kulipa mishahara na posho za waajiriwa. Jedwali 4.4, Umbo 4.4.1 na Umbo 4.4.2 yameainisha idadi na mgawanyo wa waajiriwa katika makundi mbalimbali.

*Jedwali 4.4 Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa*


| Kundi | Watanzania Walioajiriwa | Wageni Walioajiriwa | Watanzania Wanaojitolea | Wageni Wanaojitolea | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| Vijana | 7,315 | 24 | 5,248 | 277 | 12,864 |
| Watu Wazima | 5,839 | 92 | 2,586 | 153 | 8,670 |
| Wazee | 102 | 3 | 54 | 8 | 167 |
| **Jumla** | **13,256** | **119** | **7,888** | **438** | **21,701** |

### *Umbo 4.4.1: Mgawanyo na Idadi ya Waajiriwa*




| | Watanzania walioajiriwa | Wageni walioajiriwa | Watanzania wanaojitolea | Wageni wanaojitolea |
|---|---|---|---|---|
| Vijana | 7,315 | 24 | 5,248 | 277 |
| Watu Wazima | 5,839 | 92 | 2,586 | 153 |
| Wazee | 102 | 3 | 54 | 8 |

### *Umbo 4.4.2: Mgawanyo wa Ajira kwa Jinsia*




Uchambuzi unaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyoongoza kwa kutoa ajira ni pamoja na Shirika la Village Schools Tanzania (702), Shirika la World Vision Tanzania (536), Shirika la Brac Maendeleo Tanzania (451), Shirika la Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania – CCBRT (403), Shirika la Danish Refugees Council – DRC (320), Shirika la Amref Health Africa – Tanzania (289),

Shirika la African Relief Organization (238), Shirika la Marie Stopes Tanzania (212), Shirika la Foundation for African Medicine Education (176) na Shirika la Medical Teams International (162).

## 4.5 Makato ya Kisheria ya Posho na Mishahara ya Waajiriwa

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba 2023, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 205 yalichangia kiasi cha Shilingi 42,603,379,942 kupitia Kodi ya Mishahara (PAYE), Mashirika 267 yalichangia kiasi cha Shilingi 30,873,522,541 kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Mashirika 112 yalichangia kiasi cha Shilingi 2,816,947,325 kupitia Kodi ya Ujuzi (SDL) na Mashirika 240 yalichangia kiasi cha shilingi 1,154,751,310 kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Aidha, uchambuzi unaonesha kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyofanya vizuri ni pamoja na Shirika la Amref Health Africa – Tanzania, Shirika la Tanzania Health Promotion Support (THPS), Shirika la World Vision Tanzania, Shirika la JHPIEGO Corporation, Shirika la Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT), Shirika la Compassion International Inc., Shirika la Plan International, Shirika la World Wide Fund for Nature – WWF, Shirika la Program for Appropriate Technology in Health (PATH) na Shirika la Pathfinder International.

## 4.6 Utekelezaji wa Sera za Ndani ya Uendeshaji wa Mashirika

Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001), pamoja na mambo mengine, inaweka misingi ya uwazi na uwajibikaji, ambapo pamoja na mambo mengine inayataka Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa na Sera na Kanuni za Ndani ili kuimarisha misingi ya uwazi, uwajibikaji, uadilifu na uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Aidha, Kanuni ya 14 ya Kanuni Na. 609 ya mwaka 2018 na Kanuni ya 6 (1) (e) ya Kanuni Na. 363 ya mwaka 2008 imesisitiza uwepo wa sera hizo ili kuhakikisha uzingatiaji wa misingi ya uwazi na uwajibikaji na kuepuka mgongano wa kimaslahi. Sera na Kanuni hizo ni pamoja na Sera ya Ajira, Sera ya Fedha, Sera ya Manunuzi, Sera ya Jinsia, Mipango na Mikakati ya muda mrefu, wa kati na mfupi.

Uchambuzi unaonesha kuwa kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 24 yaliyofanyiwa uhakiki, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 18 yalibainika kuwa na Sera na Kanuni za Ndani za uendeshaji. Tathmini inaonesha kuwa idadi hiyo ni sawa asilimia 75 ya Mashirika ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yaliyobainika kwa na Sera hizo.

# SURA YA TANO

## Changamoto na Mapendekezo ya Kuboresha Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali

### 5.1 Utangulizi

Serikali ya Tanzania inatambua kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni mdau mkubwa wa maendeleo nchini na kwamba yamekuwa yakifanya kazi kubwa ya kujenga uwezo kwa wananchi hasa katika kutambua haki na wajibu katika kujiletea maendeleo kiuchumi na kijamii. Katika kufanikisha masuala hayo, kazi kubwa ya Serikali ni kujenga mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yake ufanisi.

Aidha, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama mdau muhimu wa maendeleo ya Taifa yameendelea kutoa mchango mkubwa ambao unaonekana kupitia fursa mbalimbali za ajira, pamoja na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali katika sekta za afya, uwezeshaji wa jamii kiuchumi, kilimo, elimu, maji, ulinzi wa jamii, uhifadhi wa mazingira, haki za binadamu, utawala bora na maendeleo ya jinsia.

### 5.2 Changamoto

Kufuatia uchambuzi wa taarifa za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa mwaka 2023, pamoja na majadiliano yaliyofanywa na wawakilishi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali wakati wa zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya miradi iliyofanyika katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Njombe, Kilimanjaro, Mwanza, Morogoro, Singida, Tabora na Tanga, baadhi ya changamoto zilizobainika ni pamoja na:

(a) Baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutowasilisha taarifa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, ambapo kati ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 7,931 yaliyotakiwa kuwasilisha taarifa, ni Mashirika 1,368 tu ndio yaliwaisilisha taarifa hizo. Kutowasilisha taarifa hizo kunapunguza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa.

(b) Baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kushindwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS) kwa usahihi na hivyo kuwasilisha taarifa ambazo hazijakamilika. Hali hiyo imekuwa ikisababisha kukosekana kwa taarifa sahihi za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na hatimaye kushindwa kabisa kutambua mchango wa Mashirika husika.

(c) Changamoto ya upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, ambapo baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakitekeleza shughuli zao kwa bajeti finyu. Aidha, vigezo na Masharti ya baadhi ya wafadhili vinakwamisha utekelezaji wa miradi na afua mbalimbali za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

(d) Ushirikiano hafifu kutoka kwa jamii imebainika kuwa miongoni mwa changamoto zinakwamisha uendelevu wa miradi inayotekelezwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kuwa baadhi ya makundi katika jamii yanamiini kuwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakipata fedha nyingi kutoka kwa wafadhili.

(e) Baadhi ya kodi zinazotozwa kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA) zimetajwa kuwa sio rafiki kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Kwamba, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yamekuwa yakitozwa kodi hizo sawa na zinavyotozwa kwa Makampuni.

(f) Kukosekana kwa ujuzi mahsusi kwa ajili ya kuyawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuandaa vyema maandiko ya miradi ya ufadhili (project funding proposals). Kwamba, kukosekana kwa ujuzi mahsusi kumesababisha baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kukosa fursa mbalimbali za ufadhili zinazotolewa na washirika wa maendeleo na sekta binafsi.

## 5.3 Mapendekezo

Kwa kuzingatia changamoto mbalimbali zilizobainishwa katika taarifa hii, mapendekezo yafuatayo yametolewa ili kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazoyakabili Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hapa nchini na hatimaye kuboresha uratibu na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali:

(a) Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kuendelea kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau mbalimbali kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili na Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NIS), sambamba na kuhamasisha uwasilishaji wa taarifa ili kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali.

(b) Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na wadau wengine watumie huduma zinazotolewa na Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi (Tax Ombudsman Service Tanzania - TOST), ambayo ina jukumu la kupitia na kushughulikia malalamiko yote ya walipakodi kuhusu huduma, masuala ya kiutaratibu na kiutawala yanayoweza kujitokeza katika usimamizi wa sheria za kodi kwa usawa na maridhiano.

(c) Serikali kupitia Wizara, Idara na Taasisi zake iendelee kujenga, kuimarisha na kuboresha mazingira wezeshi kwa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kukua, sambamba na utoaji wa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia shughuli za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

(d) Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa iendeleze utaratibu wa kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika masuala mbalimbali, ikiwemo uandishi wa miradi ya ufadhili na kuweka utaratibu maalum wa kuyaunganisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wafadhili.

(e) Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) iendelee kuyahamasisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya Kimataifa na Mashirika makubwa kuyajengea uwezo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani na yenye uwezo mdogo kama ilivyoainishwa katika Kifungu cha 31(c) cha Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

## 5.4 Hitimisho

Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali itaendelea kujenga na kuimarisha mazingira wezeshi ya utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali.

Kwa upande mwingine, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yana jukumu la kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ya uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, kuimarisha misingi ya uwazi, uwajibikaji na uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, pamoja na kuongeza utambuzi wa mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika nyanja mbalimbali za maendeleo.

# REJEA

**JMT** 1996. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Jamii, 1996. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

**JMT** 1999. Mkakati wa Kitaifa wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Kitengo cha Uratibu.

**JMT** 2022. Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2022/2023 - 2026/2027 (MKIUMA).

**JMT** 2001. Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, 2001. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

**JMT** 2002. Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 ya mwaka 2002. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

**JMT** 2002. Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake, 2023. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

**JMT** 2013. Mpango wa Kitaifa wa Haki za Binadamu, 2013-2017, Wizara ya Katiba na Sheria

**JMT** 2004. Kanuni ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Tangazo la Serikali Na. 152, 2004. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

**JMT** 2020. Mwongozo wa Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara, 2020. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

**JMT** 1977. Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, 1977. Wizara ya Katiba na Sheria.

**JMT** 2003. Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii, 2003. Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu

**JMT** 2014. Sera ya Elimu na Mafunzo, 2014. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**JMT** 2021. Sera ya Taifa ya Mazingira, 2021. Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira.

**JMT** 2021. Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26. Wizara ya Rais – Mipango na Uwekezaji.

**JMT** 2013. Sera ya Taifa ya Kilimo, 2013. Wizara ya Kilimo.

**JMT** 2002. Sera ya Taifa ya Maji, 2002. Wizara ya Maji.

**JMT** 2007. Sera ya Afya, 2007. Wizara ya Afya




## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

**Simu Na:** 255 (026) 2963341/2963346
**Nukushi:** 255 (026) 2963348
**Barua Pepe:** ps@jamii.go.tz
**Tovuti:** www.jamii.go.tz

**Mji wa Serikali - Mtumba,**
Mtaa wa Afya,
S. L. P 573,
40480 DODOMA.